

unalenga kurejesha kwa jamii ambapo benki hiyo inafanyia kazi.

"Tunafuraha kukabidhi madawati na meza kwa shule tatu katika Wilaya ya Ifala

Sekondari ya Tambaza, Hussein Mavunua aliipongeza benki hiyo kwa kusaidia maendeleo ya shule kwa miaka mingi sasa na kuongeza kuwa.

LIHURU UK 7.

Ulega aja na kopa ng'ombe lipa maziwa

Kagera

NA MWANDISHI WETU

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mary Chatanda, ameipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuazisha programu ya kopa ng'ombe lipa maziwa yenye lengo la kuwawezesha vijana kujiimarisha kiuchumi.

Akizungumza jana katika ziara ya Mwenyekiti wa UWT Taifa, Chatanda alisema fursa hiyo ni nzuri kwani program hiyo itawahakikishia vijana hususan wanawake kuimarika kiuchumi kupitia sekta ya mifugo.

"Wizara imepata waziri kijana ambaye ana uwezo mkubwa wa kuhakikisha malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita yanatimia kwa upande wa Mifugo na Uvuvi na wananchi wanafurahia matunda hayo.

Aliongeza kuwa: "Wanufaika wa program hii wapo 58,747 ambapo

wanawake 17,545 wakiwemo vijana 624 katika Mkoa wa Kagera, niwaombe muendeleo kuwapa fursa hiyo zaidi wanawake na vijana ili wajiinue zaidi katika uchumi."

Chatanda alishauri usimamizi wa ng'ombe hao kupewa kipaumbele pamoja na vijana wanaowezeshwa kupitia program hiyo kupewa elimu zaidi itakayowafanya kunufaika zaidi kiuchumi.

Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alimshukuru Mwenyekiti Chatanda kwa kuendelea kutoa elimu katika maeneo yote nchini ikiwemo Mkoa wa Kagera kwa kuwa ziara ya UWT Taifa itawaelewesha wanawake kuchangamkia fursa hiyo.

Ulega alisema serikali ipo kwa ajili ya kinamama na vijana katika kuhakikisha wanapewa fursa za kiuchumi, hivyo niwaombe wanawake na vijana kuchangamkia fursa hiyo muhimu kiuchumi.